

## ADAMU

Adamu alikuwa mwanzilishi wa kweli: yeye alikuwa mtu wa kwanza duniani na nabii wa kwanza! Aliifundisha familia yake injili, lakini hata mwanzo, wengi "walitafuta ushauri wao wenye gizani" na kuukataa ukweli (Musa 6:28).

## HENOKO

Je, umewahi kusikia juu ya mji wote kuchukuliwa kwenda mbinguni? Vema, mji wa Sayuni—ulianzishwa na Henoko—ulikuwa wa haki zaidi kwamba watu wake walienda kukaa na Mungu (ona Musa 7:23).

## NUHU

Unajua kuhusu safina ya Nuhu. Watu wanane tu—familia ya Nuhu—walinusurika na Mafuriko kwa sababu walisikiliza maonyo ya Nuhu (ona Mwanzo 7; Musa 8). Lakini ulijua kwamba alipokea ukuhani alipokuwa na umri wa miaka 10 (ona M&M 107:52) na kwamba "mapandikizi ya watu... walimtafuta Nuhu ili wamtoe uhai wake"? Musa 8:18.

## WAKUU WA VIPINDI VYA MWONGOZO WA MUNGU

Manabii hawa waliitwa na Mungu, "kwa ajili ya imani yao kuu na matendo yao mema" (Alma 13:3; ona pia Ibrahimu 3:22–23). Funguo za ukuhani walizoshikilia zilirejeshwa kwa Nabii Joseph Smith. Haya ni mambo machache ya kuvutia kuhusu manabii hawa. Angalia kitu kingine unachowenza kujifunza kuhusu wao unapojifunza maandiko.

## IBRAHIMU

Ibrahimu alikuwa karibu atolewe kafara na makuhani waovu, lakini malaika alimuokoa (ona Ibrahimu 1). Alipata baadhi ya ufunuo wa kupendeza, ikijumuisha ono la maisha kabla ya kuja duniani. Waumini wa Kanisa ni uzao wake, na agano la Ibrahimu limepewa jina kutoka kwake. (Ona Ibrahimu 2–5.)

## MUSA

Musa aliwaongoza Waisraeli kutoka Misri na kuwasaidia kupata uhuru wao. Yeye "alitafuta kwa bidii kuwatakasa watu wake ili kwamba wauone uso wa Mungu; lakini walifanya miyo yao kuwa migumu na hawakuweza kustahimili uwepo wake" (M&M 84:23–24). Hakika, kwa sababu ya ukengefu wao, walitangatanga nyikani kwa miaka 40!

40

## YESU KRISTO

Sio tu kwamba Yesu Kristo alifundisha injili na kufanya miujiza mingi, lakini pia alianzisha Kanisa Lake duniani. Yeye alilipia adhabu ya dhambi zetu na alisulubiwa na kufufuka ili kutuwezesha sisi kushinda kifo cha kiroho na cha kimwili. Yeye ndiye kichwa cha Kanisa Lake leo, na Yeye na Baba wa Mbinguni ni chanzo cha mamlaka ya ukuhani.

## KUTENGENEZA UPYA

Wakati wa Ukengefu Mkuu, baadhi ya watu wenye mawazo ya-kidini huko Ulaya waligundua kwamba injili ya Yesu Kristo haikuwa ikifundishwa kwa usahihi. Watengenezaji upya hawa hawakuwa manabii, lakini walifanya kwa kadri ya uwezo wao kufundisha ukweli jinsi walivouelewa. Walisaidia kufanya Biblia ipatikane kwa watu wengi zaidi. Wengi walipigania uhuru wa dini na kufungua njia kwa ajili ya Urejesho wa injili.

## UKENGEUFU MKUU

Baada ya Ufufuko wa Mwokozi, Mitume Wake na viongozi wengine wa Kanisa walijaribu kuieneza injili, lakini watu walikataa mafundisho yao na hata kuwaa Mitume wengi. Kwa sababu ya uovu wa watu, utimilifu wa injili ulipotea duniani. Ulimwengu uliangukia kwenye giza la kiroho (ona Isaya 60:2).

- Kwa zaidi ya miaka 1,000, watu hawakuweza kupata ibada za wokovu, baraka za hekaluni, au mwongozo wa nabii.
- Ukweli wenye thamani ulipotea kutoka kwenye Biblia.
- Dhana za uongo zilifundishwa kuhusu ukweli juu ya asili ya Mungu.
- Baadhi ya ibada za wokovu zilibadilishwa au kufundishwa visivyo sahihi (ona Isaya 24:5).
- Ukengefu huu hatimaye ulileta kuanzishwa kwa makanisa mengi.

## JOSEPH SMITH

Hivyo utimilifu wa injili ulikuwa umepotea milele? La! Mungu alifunua ukweli muhimu kwa Joseph Smith tena. Wajumbe wa Mbinguni walirejesha kwake funguo zote muhimu za ukuhani (ona M&M 27:8–13; 110; 128:18–21), zikifanya hiki kuwa "kipindi cha mwongozo wa Mungu cha utimilifu wa nyakati" (M&M 138:48). Pia kinajulikana kama siku za mwisho kwa sababu ni kipindi cha mwisho cha mwongozo wa Mungu kabla ya Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.

*We we  
Uko  
Hapa*

## UREJESHO

Je, unajua? WEWE una baraka za Urejesho. Ndiyo, wewe!

- Kanisa la Yesu Kristo lilirejeshwa likiwa na nabii na mitume ili kuliongoza.
- Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, Lulu ya Thamani Kuu, na ufunuo mwininge wa kisasa vilirejesha ukweli wa thamani uliokuwa umepotea (ona 2 Nefi 27).
- Joseph Smith alipokea Ukuhani wa Haruni kutoka kwa Yohana Mbatizaji (ona M&M 13) na Ukuhani wa Melkizedeki kutoka kwa Petro, Yakobo, na Yohana (ona M&M 128:20).
- Wenye ukuhani waliopewa mamlaka hufanya ibada za wokovu kwa usahihi.
- Na tunajua kwamba ukweli kamwe hautaweza kupotea kwa njia ya ukengefu tena (ona Danieli 2:44). ■